



# JOHN MERLINI SECONDARY SCHOOL

MISSIONARIES OF THE PRECIOUS BLOOD  
P.O. Box 2010  
DODOMA - TANZANIA

tel. 0766 939 536  
e-mail: [jmerlinisec@gmail.com](mailto:jmerlinisec@gmail.com)  
web-site: [cppseducation.sc.tz](http://cppseducation.sc.tz)

Registration N° S 4880, NECTA Exams N° S 5391

## FOMU YA OMBI LA KUJIUNGA NA SHULE MWAKA 2025

Picha  
Yako

Shule ya Sekondari ya John Merlini ipo Miyuji, Jijini Dodoma. Inamilikiwa na Shirika la Wamisionari wa Damu Azizi. **Ni shule ya mseto, (wasichana na wavulana) ni ya bwani.** Ni shule inayofanya vizuri kitaaluma na malezi ya watoto. Kitaaluma daima ipo kwenye tatu bora za Mkoa wa Dodoma.

Fomu hii kwa Dodoma inapatikana shuleni John Merlini na katika Parokia za Kisasa, Nkuhungu, Kazimoto Plaza na Radio Mwangaza. Kwa Dar es Salaam inapatikana Parokia za Tegeta, Boko, Bahari Beach, Kunduchi Mtongani, St. Gaspar-Mbezi Beach. Pia fomu inapatikana Msimbazi centre No 09 na 22 na kwenye website yetu.

Gharama ya fomu ni **sh. 20,000/=** na ilipwe kwa njia ya Benki.

- JINA LA BANK : **NMB**
- JINA LA ACCOUNT : **JOHN MERLINI SECONDARY SCHOOL**
- NAMBA YA ACCOUNT : **52010026469**

Mtihani wa kujiunga na shule (entrance test), utafanyika shuleni John Merlini (Dodoma), kwa Dar es Salaam Parokia ya St. Nicholas Kunduchi Mtongani siku ya Jumatatu tarehe **16/09/2024** kuanzia saa 1:30 asubuhi. Masomo ya ushahidi ni **Hesabu, Sayansi na English. KIPAUMBELE KITAKUWA KWA WATAKAOFAULU ZAIDI.**

Masomo ya Pre – Form one ni lazima kwa wale waliochaguliwa kujiunga na shule. Pre-Form one itaanza tarehe **14/10/2024** hadi tarehe **30/11/2024**. Wote pia wanapaswa kukaa Bwani. Gharama ya Pre- Form one kwa muda huo ni **Tshs. 400,000/=** Gharama hii nayo ilipwe kwa njia ya Bank.

Ada ya shule ni **shs. 2,300,000 (Milioni mbili na laki tatu tu)**, Michango inayochangishwa na serikali haipo ndani ya ada. Ada inaweza kulipwa kwa awamu moja (January siku shule inapoanza) au awamu mbili (January na July) au awamu tatu (January, Aprili, July) na awamu nne kwa wanafunzi wa kidato cha kwanza na cha tatu (Kila baada ya likizo).

**Mwanafunzi aje na fomu hii ikiwa imeambatanishwa na picha na pay in slip ya Benki siku ya mtihani. Mwanafunzi atatakiwa pia kuvaa sare ya shule alikomaliza shule ya msingi anapokuja kufanya mtihani.**

### **MAELEZO:**

Jina la Mwanafunzi .....

Jina la Mzazi/Mlezi .....

Tarehe – Mwezi – Mwaka wa kuzaliwa .....

Mwaka wa kumaliza elimu ya msingi .....

Namba ya mtihani wa Darasa la VII .....

Shule alipomalizia Darasa la VII .....

Simu ya Mzazi/Mlezi wako .....